**HOTUBA YA UTANGULIZI YA MHE. SALIM AHMED SALIM, MWENYEKITI WA TAASISI KATIKA UZINDUZI RASMI WA MPANGO KABAMBE WA KUISAIDIA NA KUICHANGIA TAASISI YA MWALIMU NYERERE FEDHA NA MALI NYINGINE KATIKA UKUMBI WA DIAMOND JUBILEE TAREHE 09.03.2002**

---

Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mgeni wetu Rasmi na Mama Anna Mkapa,

Mama Maria Nyerere,

Waheshimiwa Wageni wetu Maalum,

Waheshimiwa Mawaziri,

Waheshimiwa Mabalozi,

Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa,

Waheshimwa Viongozi wa Taasisi mbalimbali,

Waheshimiwa Wageni Waalikwa,

Mabibi na Mabwana.

Naomba kuanza kwa kutoa shukrani zetu za dhati kwako Mheshimiwa Rais kwa kukubali ombi letu kuwa Mgeni Rasmi katika shughuli hii. Kuwepo kwako hapa ni kelelezo sahihi juu ya umuhimu unaoipa Taasisi ya Mwalimu Nyeree katika kuyaendeleza yale mambo ya msingi ambayo Marehemu Baba wa Taifa letu aliyasimamia na kuyaendeleza. Kukubali kwako kuwa Mgeni Rasmi pia kumeipa shughuli hii umuhimu wa peke yake. Vile vile napenda kuwashukuru wageni wetu maalum pamoja na wageni wetu wote waliohudhuria hapa. Tunathamini sana kufika kwenu hapa.

Taasisi ya Mwalimu Nyerere ilianzishwa rasmi Juni 1996, kwa heshima ya Baba wa Taifa, na iwe kumbukumbu ya kazi kubwa aliyoifanya katika maeneo mbalimbali ya kutetea wanyonge, kutetea, kulinda na kuimarisha Umoja na Amani ndani ya Taifa letu na katika bara la Afrika kwa jumla na pia kuimarisha mshikamano katika Dunia ya tatu yaani nchi zinazoendelea kama ni sehemu ya kuimarisha uelewano, amani na mshikamano duniani. Hayo yote Mwalimu aliyafanya kama Kiongozi Mkuu wa Tanzania na pia kwa upande wa bara letu alifanya hivyo kwa kushirikiana na viongozi wenzake.

Itakumbukwa kwamba Mwalimu katika uhai wake alisisitiza sana suala la Amani na Umoja kwani alielewa fika kwamba hiyo ni misingi madhubuti ya kuhakikisha utulivu na

maendeleo ndani ya nchi yetu na ndani ya bara letu. Kwa mfano Mwalimu alisema maneno yafutayo mwaka 1987 kuhusu Amani na Umoja hapa Tanzania naomba kununukuu:

> "Kwa nchi yoyote duniani Umoja na Amani ni nguvu kubwa. Kwa nchi changa na maskini kama nchi yetu, Umoja na Amani ni Amana na Tunu kubwa isiyo na bei. Tukiulizwa na wenye kiburi na fidhuli ya wingi wa mali: Mna nini, ninyi Watanzania? Tunaweza kujibu, si kwa fidhuli, lakini kwa fahari kabisa: tuna Umoja na Amani; vitu ambavyo havinunuliki kwa kiasi chochote cha fedha. Tuna haki ya kujivunia Umoja huu na Amani hii, maana ndivyo vilivyotuwezesha kupambana na matatizo makubwa ya vita, ya uchumi, na hata ya kisiasa. Tuna haki ya kujivuna kwa sababu Umoja huu na Amani hii havikuzuka vyenyewe tu: mbona havizuki kila mahali? Wahenga wamesema: *'ukiona vinaelea vimeundwa'*."

Shughuli iliyotukusanya hapa ni kuchangia, kwa hiari ya kila mmoja wetu, na kila kundi ili kuiwezesha Taasisi kushughulikia mambo ya Amani na Umoja wa Taifa letu, Afrika, na ushirikiano katika Dunia. Amani na Umoja tulio nao Tanzania ni mali ya Watanzania wote – ni Amana na Tunu

kubwa isiyo na bei. Watanzania wote tunajivunia Amani na Umoja wetu – tunayo haki na tunazo sababu nzuri za kujivuna na kujipongeza. Kila tukifanya hivyo, tunajikumbusha kuhusu mafanikio yetu, na msingi wa nguvu kubwa ya Watanzania wote.

Vyombo vingi, na watu wengi binafsi, wamefanya kazi kubwa ya kujenga na kuimarisha Amani na Umoja wetu – Vyama vyetu vya Siasa vya awali: TANU na Afro-Shiraz; na baadaye CCM; Vyama vya Ushirika, Wazazi, Wafanyakazi, na leo Vyama vipya vya Siasa vilivyozaliwa baada ya mabadiliko ya 1992. Viongozi wengi kama vile Rais wa Kwanza wa Zanzibar Hayati Sheikh Abedi Amani Karume na wenzake, Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius K. Nyerere na wenzake wote na Viongozi wengine wengi wa fani mbalimbali, wamefanya kazi nzuri iliyotukuka, na inayostahili kukumbukwa na kuheshimiwa na sote tuliopo hapa, na wale wasiokuwapo.

Mafanikio ya juhudi zote hizo vimetokana na mambo mawili makubwa: Kwanza ni uamuzi wa makusudi wa viongozi waanzilishi wa Taifa letu, wa kuzingatia misingi muhimu ya maisha ya binadamu. Imani katika **usawa wa binadamu** wote, katika kuheshimu **utu** wa kila mtu, katika **uhuru** wa mtu binafsi na **uhuru** wa jamii nzima katika kujitoa mhanga **kuwatumikia** binadamu wengine bila kubagua kwa misingi ya kabila, dini, rangi, jinsia, asili au atokako mtu na katika

maendeleo yanayowanufaisha watu wote. **Pili** ni uamuzi wa makusudi wa kuwapa Watanzania wote nafasi ya kushiriki katika maamuzi ya mipango na utekelezaji wa mipango ya maendeleo yao. Tangu awali kabisa baada ya Uhuru wa Tanzania Bara 1961 na Muungano wa 1964 Watanzania wamejitahidi kuwa na **uongozi wa pamoja,** ukishirikisha vyombo vyote vya dola na Wananchi wa ngazi zote. Utaratibu huu umetuwezesha kufahamiana vizuri, kutegemeana, kuaminiana na kusaidiana wakati wote.

Msingi wa Amani na Umoja ni Haki; iwepo haki au matumaini ya kujenga Haki katika Taifa na miongoni mwa raia. Pale ambapo hapana Haki, wala matumaini ya kujenga Haki, Amani na Umoja ni ndoto, na mwisho wake ni fujo, lawama, mgawanyiko, mapambano na hata vita. Kuwepo haki pia kunahitaji mapambano ya kudumu dhidi ya rushwa na matumizi mabaya ya madaraka. Pia kunahitaji utawala bora. Vyinginevyo ni kupalilia matatizo na shari. Afrika inayo mifano mingi sana ya hali hiyo. Safari ya kwendea jamii ya haki na usawa ni ndefu na si nyepesi. La msingi ni kwamba tuendelee kupiga hatua muhimu na imara kufikia lengo hilo.

Taasisi hii inatetea na kupigania **haki** maana Amani na Umoja haviwezekani pale ambapo haki inapindwa, kupigwa vita, au kupuuzwa kabisa. Haki na maisha ya haki, ndiyo mama wa Amani na Umoja. Sumu ya Amani na Umoja ni kuendekeza

ubaguzi wa kila aina, uwe wa dini, jinsia, elimu, rangi, ukabila, eneo, kimo au hata sura; kupuuza utu wa kila mtu, na mahitaji muhimu ya utu huo – chakula, malazi bora, elimu, mavazi, uhuru na maendeleo ya jumla yenye tija. Watanzania wanathamini sana utu, uhuru wa kila mtu na ule wa Taifa lao; wanatambua na kuukubali usawa wao kama watu wenye vipaji tofauti wanaoweza kuhitilafiana bila kupigana; au kupigana kisha wakazungumza; na wanaotumia tofauti za vipaji vyao kuimarisha misingi ya Amani na Umoja wao. Moja ya kazi za Taasisi ni kulinda misingi hii na kuitetea na kuihubiri wakati wote miongoni mwa Watanzania na Waafrika pia.

Amani na Umoja ndani ya nchi yetu na katika bara letu ndiyo mradi mkubwa sana wa Taasisi hii. Kushirikiana na Watanzania, Serikali zao, Taasisi zao za kiraia za aina zote, ni moja ya mbinu ya utendaji wa Taasisi. Kuandaa na kuwezesha mazungumzo ya mara kwa mara baina ya watu, miongoni mwa watu, na kati ya watu na vyombo vyao vya utawala, ili kujenga uwezo wa kushughulikia matatizo yao ni moja ya kazi za Taasisi ya Mwalimu Nyerere. Mfano mmoja wa shughuli za Taasisi hii katika kupigania Amani na Umoja ndani ya Afrika ni kazi ya usuluhishi iliyofanywa kuhusu Warundi kule Arusha chini ya Uongozi wa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius K. Nyerere na mwavuli wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere. Katika upeo huo huo wa kuimarisha Umoja

na Amani, Taasisi ilipata faraja kubwa kwa muafaka uliopatikana baina ya Vyama vya CCM na CUF. Tunawapongeza Viongozi wa Vyama hivyo kwa hatua hiyo muhimu na ya kihistoria yenye maslahi ya Taifa letu na bara letu. Pongezi za ziada zinakwenda kwako Mheshimiwa Rais pamoja na Rais wa Zanzibar kwa uamuzi wenu na vitendo vyenu vya kusimamia kikamilifu utekelezaji wa muafaka huo.

Kama Watanzania na kama Waafrika tunahitaji, na tunalazimika kuendela kuimarisha na kudumisha Amani na Umoja ndani ya nchi yetu na ndani ya bara letu ili tupate nguvu za kuishi kwa ushindani katika dunia ya leo. Dunia ya leo haina huruma; wala si dunia ya mchezo mchezo. Yapo mashindano makali siku hizi ya elimu, teknolojia na uchumi. Mataifa makubwa yanashindana vikali yenyewe kwa yenyewe, lakini pia yanajenga uwezo wa umoja, kama ule wa Umoja wa Ulaya, wanaoutumia kama mbinu na nyenzo ya kushindania. Hao ni wakubwa; ikiwa wao wanataka Amani, na wanaimarisha Umoja wao sembuse sisi! Sisi wadogo tunahitaji zaidi Amani na Umoja ili tujenge na kuimarisha nguvu zetu za kujilinda, kujitetea na kushindana katika Dunia hii ya **utandawazi**.

Mheshimiwa Rais, leo siyo siku ya hotuba ndefu ni siku ya kuchangia. Naomba kumalizia kwa mara nyingine tena kutoa shukrani nyingi sana kwako binafsi, na kwa wageni wetu

wengine wote kwa kuja kuiunga Taasisi mkono. Tunafurahi kwamba mmekuja hapa kwa wingi, upendo na hiari, ili kwa pamoja tuichangie amani yetu na umoja wetu. Taasisi ya Mwalimu Nyerere ni mali yetu sisi sote. Ni Taasisi ambayo kwa historia yake na malengo yake ni kwa maslahi ya Watanzania wote. Ni Taasisi inayohitaji ushirikiano na michango ya wote wale wanaoamini yale yanayosimamiwa bila ya kujali wana imani na Chama gani cha siasa au hata kama hawako kabisa katika Vyama vya Siasa. Hii ni Taasisi ambayo Baba wa Taifa letu, akiwa hai, alituriithisha kwa sahihi yake, ili tuitumie kulinda, kuimarisha na kudumisha Amani na Umoja katika Tanzania, Afrika na Duniani kote.

Naomba kumalizia kwa kutoa shukrani zetu za dhati kwako wewe Mheshimiwa Rais, kwa jinsi ulivyoisaidia Taasisi yetu - kimawazo na kwa vitendo. Tunathamini sana mchango wako na tuna imani kwamba utaendelea kutusaidia ili tufanikishe malengo muhimu ya Taasisi hii kama yalivyoainishwa na Marehemu Baba wa Taifa letu.

Ahsanteni kwa kunisikiliza.